Africa Journal of Language Studies (AJLS)
Vol. 1 Issue 1 | [November] [2024] | [Page 64] – [Page 75]
Journal homepage: https://ajls.kab.ac.ug
ISSN: 3078-4301

# Miktadha ya Kisintaksia itokanayo na Makusudio ya Mawasiliano katika Uibuzi wa Miundo Virai Kubalifu ya Kiswahili

**Musa .O. Amanzi**[1]
[1] Muslim University of Morogoro, Tanzania
*amanzimussa2020@gmail.com*

---

**Article History:**
**Received:** 15 Aug 2024
**Accepted:** 21 Oct 2024
**Published:** 11 Nov 2024

**Maneno muhimu:**
Miktadha ya Kisintaksia; Makusudio ya Mawasiliano; Uibuzi wa Miundo Virai Kubalifu

*This is an open access article under the CC-BY-NC-ND license*

## Ikisiri

Lugha ya Kiswahili ni lugha yenye muundo wa kitenzi kati yaani, katika sentensi ni lazima kuwe na viambajengo kabla au baada ya kitenzi ambavyo vinaweza kuwa dhahiri au visiwe dhahiri. Kuwapo kwa muundo huu hakumaanishi kuwa lugha hii ina utaratibu mmoja kiusemaji. Bali, ipo miundo mingine ambayo kimsingi ujitokezaji wake husababishwa na miktadha mbalimbali ya kisintaksia. Makala haya kwahiyo yanalenga kuchunguza miktadha ya kisintaksia itokanayo na makusudio ya mawasiliano katika uibuzi wa miundo virai kubalifu vya sentensi za Kiswahili. Data za makala hayazilipatikana uwandani kupitia mbinu ya ushuhudiaji sikizi na mahojiano. Nadharia ya Uchunguzi wa Kimaeneo ya Joshua Aaron Fishman mwaka (1972) ilitumika katika uchanganuzi na uwasilishaji wadata. Katika uwasilishaji wa kila data, alama "Mt." ilitumika ikimaanisha "mtoataarifa". Matokeo ya makala haya yanaonesha kuwa kuna miktadha sita ya kisintaksia itokanayo na makusudio ya mawasiliano katika uibuzi wa miundo virai kubali vya sentensi za Kiswahili. Miktadha hiyo ni umadaishaji, ufokasilishaji, usititizi, uulizi, maombi na kuagiza. Aidha, makala haya yanapendekeza kuwa tafiti nyingine zifanyike ili kuchunguza miundo virai kubalifu itokanayo na miktadha ya kisintaksia ya makusudio ya mawasiliano.

---

# Emergent Syntactic Contexts from Communication Intent in Phrase Structures

## Abstract

The Swahili language is an SVO word order language. The existence of this structure does not mean sentences in Swahili have only a single structure in communication. Rather, there are many internal sentence structures apart from SVO structure depending on various syntactic contexts in communication. This article is intended to examine the syntactic contexts resulting from the purpose of communication in the derivation of the Swahili syntactic structures. The data was collected from the field through observation and interview techniques. The Language and Sociocultural Theory was

used in the analysis of data. The results of this study show that there are six syntactic contexts derived from the purpose of communication. Those contexts are topicalization, focalisation, emphasis, interrogation, inquisition and instruction. This results into realization of other forms of word order in Swahili other than SVO. In addition, this article recommends further studies to investigate syntactic phrase structures resulting from the syntactic context of communicationpurposes.

**Key Words: Syntactic Contexts, Communicative Intent, Phrase Structures**

## 1.0 **Utangulizi**

Msingi wa kupeana taarifa katika lugha yoyote ile ni mawasiliano. Kavoi na Wanjala (2013) wanaeleza kuwa, mawasiliano ni kitendo cha uwasilishaji na ung'amuaji wa maana kati ya watu au jamii kwa kutumia mfumo wa ishara na miondoko iliyokubalika katika jamii mahususi. Maelezo haya yana maana kwamba, ili kupata ujumbe sahihi katika mawasiliano hapana budi kuwasilisha na kung'amua maana iliyokusudiwa yaani, kujua makusudio ya mawasiliano hayo. Msingi wa mawasiliano ni mazungumzo baina ya watu wawili au zaidi. Hivyo, katika mazungumzo ni lazima kuwapo kwa msemaji na msikilizaji kwa utaratibu maalumu wa kuwasiliana kwa lengo maalumu. Kwa hiyo, makusudio ya mawasiliano ni ile dhamira ya msemaji kwa msikilizaji katika muktadha maalumu. Kwa mantiki hii, makusudio ya mawasiliano hutawaliwa na miktadha tofauti.

Katika lugha ya Kiswahili dhana ya muktadha imeelezwa katika pande mbili tofauti, yaani fasihi na isimu. Makala haya yameangazia ufasili wa dhana ya muktadha kwa upande wa isimu. Muktadha ni ile hali inayotawala na kuelekeza matumizi ya lugha inayozungumzwa, kwa mfano mahali, wakati, hadhira, kusudio na kadhalika (taz. Massamba, 2009; King'ei, 2010; TUKI, 2013). Fasili hii inagusa moja kwa moja lengo la makala haya kwa kueleza kuwa muktadha ni kusudio. Hivyo, muktadha wa kisintaksia ni ule utumizi wa lugha unaochagiza kupatikana kwa miundo fulani ya sentensi. Katika lugha ya Kiswahili muktadha wa kisintaksia unachochewa na makusudio ya kimawasiliano. Kusudio ndilo linaloukilia ujitokezaji wa vipengele tofautitofauti vya kisarufi kwenye tungo. Tazama mifano hapo chini:

a) Mtoto anacheza mpira mara kwa mara (muundo wake ni KN + KT (KN, KE (KH)

b) Mtoto anacheza mara kwa mara mpira (muundo wake ni KN + KT (KE (KH), KN)

c) Mara kwa mara mtoto anacheza mpira (muundo wake ni KE (KH), KN + KT (KN)

**Chanzo: Amanzi (2021)**

Ukichunguza mifano hapo juu utabaini kuwa kiambajengo mara kwa mara kimejitokeza kwa namna tofauti katika sentensi a, b, na c. Katika muktadha wa kisintaksia hizo ni sentensi tofauti kwa sababu hazikubeba kusudio moja la kimawasiliano. Hivyo, makusudio ndiyo msingi wa kuwapo kwa miundo mingi ya sentensi yenye dhamira tofauti. Kwa kuwa utafiti huu umejiegemeza katika miktadha ya kisintaksia, sentensi ndizo zimetumika kuweka bayana makusudio ya mawasiliano.

## 2.0 **Kiunzi cha Nadharia**

Makala haya yaliongozwa na Nadharia ya Uchunguzi wa Kimaeneo iliyoasisiwa na Joshua Aaron Fishman mwaka (1972) inayosema kwamba, uteuzi wa lugha hutegemeana na uzoefu wa mzungumzaji katika miktadha tofauti, tofauti ya lugha baina ya wazungumzaji, utofauti wa watumiaji lugha na utofauti wa mada ya mazungumzo. Fishman (keshatajwa) aliendelea kueleza kuwa uchaguzi wa lugha ni namna lugha ilivyoweza kutumiwa na kundi fulani la watu katika jamii kwa lengo maalumu la kuwasiliana. Kutokana na mawazo hayo ya Fishman (k.h.j), nadharia hii ina misingi ifuatayo: Mosi, lugha huelezwa kwa kuzingatia tofauti za muktadha wa mazungumzo. Pili, lugha huelezwa kwa kuzingatia tofauti za utumizi wa lugha yenyewe. Tatu, lugha huelezwa kwa kuzingatia tofauti baina ya washiriki wa mawasiliano. Nne, lugha huelezwa kwa kuzingatia utofauti wa mada ya mazungumzo na tano, uzingativu wa lengo la msemaji na mtiririko maalumu wa mazungumzo na maandishi. Hivyo basi, makala haya yaliongozwa na msingi wa tano unaosisitiza kuwa ni muhimu kuzingatia lengo la msemaji na mtiririko maalumu wa mazungumzo.

## 3.0 Methodolojia ya Utafiti

Data za utafiti huu zilikusanywa uwandani kwa wazungumzaji wa Kiswahili. Mkoa wa Morogoro ndio ulioteuliwa kama eneo la utafiti huu. Mtafiti ameteua mkoa wa Morogoro kwa sababu ni mkoa unaopakana na mkoa wa Pwani, hivyo kuna Waswahili wengi walioathirika na uswahili kutokea Pwani. Wango la utafiti huu lilikuwa ni wazungumzaji wote wa lugha ya Kiswahili ambao ni wazee wanaopatikana mkoa wa Morogoro katika vijiwe vya kahawa pamoja na wataalamu wa lugha ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro. Sampuli ya utafiti huu ilikuwa ya wazee 10 na wataalamu 5 ambao waliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Mbinuhii imetumika kwa sababu mtafiti alilenga kupata data mahususi kutoka katika vyanzo mahususi (Tavakoli, 2012).

Fauka ya hayo, data za utafiti huu zilikusanywa kupitia mbinu ya mahojiano na mbinu ya ushuhudiaji sikizi. Mbinu ya mahijiano ni majibizano ya ana kwa ana au uso kwa uso, kwa simu au barua pepe na kadhalika yanayofanywa na watu wawili au zaidi kwa lengo la kupata taarifa (Kombo, 2006). Mtafiti alitumia mbinu hii kwa sababu ilimpa uhuru wa kuuliza maswali ambayo aliyaandaa na hata ya papo kwa papo kutokana na majibu yaliyotolewa na watafitiwa wake. Hivyo,mtafiti alifanya mahojiano ya ana kwa ana na simu kwa kuwafata na kuwapigia watafitiwa wake ambao ni wazee wanaozungumza lugha ya Kiswahili. Kupitia mbinu hizi mtafiti aliweza kukusanyataarifa za kutosha ambazo zilichambuliwa na kuweza kubaini miktadha mbalimbali ya kisintaksia itokanayo na makusudio ya mawasiliano.

Mbinu nyengine, ni mbinu ya ushuhudiaji sikizi ambayo ni mbinu ya ukusanyaji taarifa ambapo mtafiti huwa katika eneo halisi la utafiti na kufuatilia jambo kwa karibu au ana kwa ana (Ponera, 2019). Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kuthibitisha matokeo ya utafiti yaliyoibuka kupitia mbinu nyingine za ukusanyaji wa data. Pia, ilimsaidia mtafiti kupata uzoefu na maarifa binafsi kwa kutafsiri yaliyoibuka uwandani badala ya kutegemea maelezo ya usaili pekee.

## 4.0 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Data za makala haya zimekusanywa kutoka uwandani kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji sikizi na mahojiano. Mtafiti alikusanya sentensi nyingi kutoka kwa wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili kwa kurekodi na kuandika baadhi kisha alitenga muda na kuzichambua. Pia, mtafiti alishirikiana na wataalamu wa lugha ya Kiswahili ili kubaini miktadha mbalimbali ya kisintaksia inayotokana na makusudio ya mawasiliano na jinsi inavyoibua miundo virai kubalifu ya sentensi za Kiswahili.

### 4.1 Miktadha ya Kisintaksia inayotokana na Makusudio ya Kimawasiliano katika Lugha ya Kiswahili

Sehemu hii inafafanua miktadha mbalimbali ya kisintaksia itokanayo na makusudio ya mawasiliano katika uibuzi wa miundo virai kubalifu ya sentensi za Kiswahili. Data za utafiti huu zilikusanywa uwandani kutoka kwa wazee wanaozungumza Kiswahili pamoja na wataalamu wa lugha ya Kiswahili. Data hizo zilifafanuliwa kwa kuongozwa na msingi wa tano wa Nadharia ya Uchunguzi wa Kimaeneo unaosisitiza kuwa, lugha huelezwa kwa kuzingatia lengo la msemaji na mtiririko maalumu wa mazungumzo na maandishi. Kupitia nadharia hii imebainika kuwa, kuna aina sita za miktadha ya kisintaksia inayotokana na makusudio ya mawasiliano yanayoukilia miundo virai

tofauti katika sentensi za Kiswahili. Miktadha hiyo ni umadaishaji, ufokasilishaji, usititizi, uulizi, maombi na kuagiza ambayo imefafanuliwa kwa undani hapa chini.

### 4.1.1 Muktadha wa Umadaishaji

Umadaishaji ni muktadha wa kisintaksia unaotokana na dhana ya kisintaksia inayoitwa mada. Kwa mujibu wa Lambrecht (1994) mada ni kiambajengo dhanilizi ambacho kinabeba taarifa ya zamani au kuukuu. Kwa kuzingatia fasili ya Lambrecht, istilahi 'mada' imetumika kwa namna mbili. Mosi, mada ni taarifa ya zamani inayojulikana katika sentensi. Taarifa hii inajulikana kwa wote yaani, mtoaji na mpokeaji wa taarifa. Aidha, taarifa hii inajulikana na inaweza kukumbukwa na mpokeaji wa taarifa kwa sababu ama imetajwa katika tungo zilizotangulia au imewasilishwa kama taarifa inayojulikana kwa kutumia mbinu za kiisimu. Pili, mada inaweza kufasiliwa kama taarifa inayoonesha sentensi inahusu nini. Kwa sababu hiyo, mada ni taarifa ambayo inapewa kipaumbele katika sentensi.

Katika sentensi, mada huwekwa mwanzoni mwa sentensi. Muktadha huu wa kisintaksia wa umadaishaji hutokana na utumizi wa viambajengo kwenye nafasi ya mwanzo katika sentensi. Kisintaksia, kiambajengo kwenye nafasi ya mwanzo ndicho kinachopewa hadhi kubwa. Ndicho kinachorejelewa na sentensi hiyo. Hivyo, kile kinachorejelewa katika nafasi ya mwanzo kwenye sentensi ndicho kilichopewa heshima ya kuwa mada katika sentensi hiyo. Kwa ujumla, muktadha wa umadaishaji ni muktadha wa kisintaksia ambao hutokana na utumizi wa viambajengo kwenye nafasi ya mwanzo katika sentensi. Tazama data ifuatayo kutoka kwa Mt. 1 kwa ufafanuzi zaidi:

*Mt.1 a). Juma anacheza mpira wa miguu*
*b). Mpira wa miguu umechezwa na Juma*
*c). Mara kadhaa, mwalimu alifungua mlango wa darasa*
*d). Kwa madaha, Asha alimtambulisha mumewe jukwaani*

**Chanzo:** Uwandani (2023)

Ukitazama data hapo juu utagundua kuwa, katika sentensi ya Mt. 1 (a) neno Juma ndilo lililoanza mwanzoni mwa sentensi (kwenye kiima), hivyohivyo kwa maneno mpira katika sentensi ya Mt. 1 (b), mara kadhaa katika sentensi ya Mt. 1 (c) na kwa madaha katika sentensi ya Mt. 1 (d). Katika sentensi zote hizo nne zina dhamira tofauti za kimazungumzo. Ujumbe sahihi unaopatikana katika sentensi hizo ni ule unaokusudiwa kurejelewa na mada hiyo. Katika sentensi ya Mt. 1 (a) kinachobeba ujumbe ni "Juma kucheza mpira". Kwa hiyo, kinachorejelewa katika sentensi hiyo ni Juma. Tofauti na sentensi ya Mt. 1 (b) kinachobeba ujumbe ni "mpira" na sio "Juma", yaani habari muhimu katika sentensi hiyo ni mpira uliochezwa. Halikadhalika, katika sentensi ya Mt. 1 (c) msisitizo ni ile hali ya kufungua mlango zaidi ya mara moja yaani ni ule ufanyaji wa kitendo kwa kufungua mlango (bila sababu). Pia, katika sentensi ya Mt. 1 (d) ujumbe unaokusudiwa ni ule umadaha katika utambulisho. Haya yote yanafafanuliwa na Nadharia ya Uchunguzi wa Kimaeneo kuwa, mpangilio wa lugha huwa unazingatia kusudio la mzungumzaji, mzungumzaji ataipamba lugha katika mtiririko ambao huweza kuendana na matarajio yake. Hivyo, data hapo juu inaonesha namna lugha inavyoweza kubeba makusudio tofauti ya wazungumzaji kupitia mtriboard wa mawazo. Hivyo, umadaishaji umejitokeza kwenye utumizi wa maneno katika nafasi ya mwanzo ya sentensi ambayo ni nafasi muhimu kisintaksia. Ukichunguza miundo ya sentensi hizo, utagundua ni miundo iliyotofautiana kutoka sentensi moja hadi nyingine, ipo miundo iliyoanza na vielezi, nomino, mnufaika na mwathirka. Kutofautiana huko ni kwa sababu muktadha wa umadaishaji huibua miundo virai tofauti ya sentensi za Kiswahili ambayo ni miundo kubalifu.

### 4.1.2 Muktadha wa Usisitizi

Kwa mujibu wa Kamusi Kuu ya Kiswahili (2022) neno usisitizi limeelezwa kuwa ni kitendo cha kukazia jambo lifanyike kwa haraka na kumalizika kwa wakati uliopangwa. Hivyo, neno usisitizi linaweza kuelezwa kuwa ni usemaji unaokazia jambo ambalo linalokusudiwa lieleweke zaidi kuliko jambo lingine. Msemaji huweza kutumia sentensi nzima kusisitiza jambo au sehemu ya sentensi. Usisitizi huweza kuwa wa namna nyingi kutegemeana na kusudio la msemaji wakati anapotaka tkusisitiza kama ifuatavyo:

#### 4.1.2.1 Usisitizi wa Uradidi

Muktadha wa kisintaksia wa usisitizi huweza kujitokeza katika uradidi wa wazi. Huu ni aina ya usisitizi ambao neno au kirai hurudiwarudiwa kwenye sentensi. Tumeuita uradidi wa wazi kwa sababu neno hurudiwa na kuonekana wazi. Katika usisitizi huu neno au kirai radidi huweza kujitokeza sehemu yoyote katika mpangilio wa sentensi. Utafiti huu umekusanya data kutoka kwa Mt. 2 zinazoonesha usisitizi wa uradidi katika mazungumzo. Kwa mfano:

*Mt. 2: Sikubali, sikubali hata aniambie nani, eti mbuzi anaweza kuzaa ng'ombe!*
**Chanzo:** Uwandani (2023)

Katika data hapo juu, msemaji Mt. 2 anarudia neno sikubali kuonesha msisitizo wa kukataa kuwa mbuzi hawezi kuzaa ng'ombe. Hapa msisitizo umewekwa kwenye kukataa kwa kutumia uradidi wa neno katika sentensi. Kwa hiyo, usisitizi huo wa kukataa umejitokeza katika hali ya ubishani. Katika data hii, inaonesha wazi kuwa msemaji anakusudia kusisitiza kukataa kwa kutumia maneno ya uradidi. Aidha, kwa kushadadia maelezo hayo, ni kwamba Nadharia ya Uchunguzi wa Kimaeneno inaeleza kuwa kila lugha ina utaratibu wake katika kueleza jambo kulingana na dhamira ya msemaji na tofauti ya muktadha wa mazungumzo.Msemaji anapokuwa katika mazungumzo huteua lugha kulingana na muktadha wa mazungumzo yake ili iweze kuendana na kusudio lake. Katika uteuzi wa namna ya kutumia lugha kulingana na kusudio la msemaji ndipo huibuka miundo mingi ya kiusemaji kama ilivyoeleza hapo juu ili kuonesha makusudio ambayo wazungumzaji hukusudia kuwasilisha. Ukirejelea data Mt. 2 mtafitiwa kwa kuwa alikusudia kukataa taarifa ambayo yeye haiamini, alisisitiza kukataa kwake kwa kurudia neno "sikubali". Hivyo, msisitizo wake ni kuoneshataarifa hiyo haipo sawa. Katika data hiyo, tunaona muundo wa sentensi unaanza na vitenzi kwa kuficha kiima.

Pia, uradidi unaweza usiwe wazi bali huweza kujitokeza viashiria ambavyo vinaonesha kuna uradidi. Kwa hiyo, uradidi unaweza ukajitokeza katika maneno ambayo yanaashiria kuwa neno hilo limeshasemwa, hivyo linarudiwa. Uradidi huu ni tofauti na uradidi wa wazi. Katika uradidi huu hakuna neno linalorudiwa bali kuna neno linaloashiria kuwa neno hilo lilishasemwa hapo awali, hivyo linarudiwa. Maneno hayo huweza kuwa vitenzi au viwakilishi virejeshi, ambavyo vinapokuwa katika sentensi huonesha uradidi wenye usisitizi wa taarifa iliyokwishasemwa. Tuchunguze uradidi unaotumia vitenzi ambavyo vinaonesha kuwa usemi unaozungumzwa ulishasemwa kabla. Katika usisitizi huu kitenzi ndicho kinachoonesha kuwapo kwa uradidi wenye usisitizi katika mazungumzo. Vitenzi hivyo ni kama vile sema, rudia, kazia na rejea vilivyobainish-wa na Mt. 2.

*Mt. 2: Nilishasema sitaki kurudi shule*
**Chanzo:** *Uwandani (2023)*

Kama data inavyonesha, taarifa ilishasemwa kabla na hapo inarudiwa tena na msemaji kutokana na uwepo wa neno nilishasema katika usemi huo. Kwa hivyo, kitenzi huweza kuonesha msisitizo wa taarifa katika mazungumzo. Kitenzi "nilishasema" kilichotumika katika data hiyo kimebeba kusudio la msemaji ambalo ni kukataa, yaani anapinga kurudi shule. Nadharia ya Uchunguzi wa Kimaeneo inaeleza kuwa mtiririko wa usemi ndiyo unaoshikilia kusudio la msemaji. Nadharia hii inaendelea kusisitiza kuwa, msingi wa kubaini kusudio la msemaji wa usemi fulani kama ni kuonya, kusisitiza au kutoa maelezo ni kuwapo kwa mtiririko maalumu wa usemi wa mzungumzaji. Katika data hapo juu, mtoa taarifa Mt. 2 anaonesha msisitizo katika makusudio ya mawasiliano yake kwa kutumia kitenzi "nilishasema" kinachoonesha uradidi wa taarifa hiyo kwa ajili ya usisitizaji. Ukichunguza muundo wa sentensi hiyo, utagundua ni muundo wa mfuatano wa vitenzi kadhaa katika tungo moja.

Aidha, usititizi huweza kujitokeza viwakilishi rejeshi. Huu ni uradidi unaotokana na viwakilishi rejeshi vinavyoonesha urudiaji wenye usisitizi wa taarifa katika sentensi. Mfano wa viwakilishi hivyo ni kama vile: hayo, hivyo na yale. Tuchunguze data ifuatayo kutoka kwa Mt. 3:

*Mt. 3: Mbona bado hamkutekeleza yale tuliyoagiza*
**Chanzo:** *Uwandani (2023)*

Katika data Mt. 3 kiwakilishi rejeshi "yale" kinaonesha kuwa kuna jambo lilielezwa kabla ili likafanyiwe utekelezaji. Hilo linabainika katika mazungumzo hayo kwa kutumia kiwakilishi rejeshi. Kutumika kiwakilishi hicho katika sentensi kinaashiria kuwa kuna wakati msemaji anaweza kurudia kusema jambo ambalo alikwishalisema kabla bila kulizungumza jambo hilo. Uwapo wa kiwakilishi "yale" ni ishara ya uradidi wenye usisitizi kuhusu jambo walilokubaliana kulifanyia kazi kabla. Hivyo, kiwakilishi rejeshi hicho kinafanya kazi ya kusisitiza kuhusu taarifa ambayo msemaji aliitoa kabla. Katika data, mtafitiwa Mt.3 anasisitiza katika maagizo aliyoyatoa huko nyuma. Haya yanadhihirika kwa kupitia mazungumzo yake aliposema "mbona bado" kisha hayo anayoyasisitiza ameyarejelea kwa kiwakilishi rejeshi "yale". Hivyo, huu nao ni sehemu ya muktadha wa usisitizi unaotokana na uradidi katika makusudio ya mawasiliano.

## 4.1.2.2 Usisitizi wa Maneno Maalumu

Muktadha wa usisitizi unaweza kujitokeza katika maneno maalumu. Huu ni usisitizi ambao hutokana na aina za maneno yenye dhima ya kusisitiza. Maneno kama nasisitiza, narudia tena, nieleweke vizuri, mmenielewa na kadhalika hutumika kusisitiza katika sentensi. Tuchunguze data ifuatayo kutoka kwa Mt. 4 ili kuthibitisha dai hili:
Mt. 4: Kutokana na utabiri wa mvua za Elinino, Rais amesisitiza wananchi wahame kutoka katika maeneo hatarishi.
**Chanzo:** Uwandani (2023)

Data ya Mt. 4 inaonesha kuwa si lazima usisitizi utumie maneno yanayojirudia; yapo maneno ambayo yanapotumiwa katika usemi fulani wa mzungumzaji hubeba dhamira ya kusisitiza. Neno "amesisitiza" katika data hiyo ni neno maalumu ambalo msemaji amelitumia kuonesha uzito wa taarifa inayotolewa. Msisitizo wa maneno maalumu hutokana na namna msemaji anavyokusudia kufikisha taarifa anayoitoa. Ufafanuzi huo unashadadiwa na Nadharia ya Uchunguzi wa Kimaeneo kuwa, ni muhimu kuzingatia lengo la msemaji na mtiririko maalumu wa mazungumzo katika kila muktadha wa kiusemaji.

Msikilizaji au msomaji hubaini kusudio kwa wepesi ikiwa tu uteuzi wa lugha umezingatiwa katika usemi uliokusudiwa. Katika data ya Mt. 4 inadhihirisha kuwa kuna muktadha wa usisitizi kwa kutumia maneno yanayoashiria wazi kuwa hapo kuna usisitizi, kwa mfano neno “alisisitiza” lilitumika katika data hiyo.

### 4.1.2.3 Usisitizi wa Vielezi Asilia

Vielezi asilia ni aina ya vielezi ambavyo havina ujazo mkubwa wa kisemantiki, huongeza maana ya kisarufi katika tungo. Vielezi asilia vinavyofanya kazi ya usisitizi ni kama vile: tena, zaidi, mno, sana na kadhalika. Tuchunguze data zifuatazo kuona utumizi wa vielezi asilia kama visisitizi vilivyobainishwa na Mt. 5:

*Mt. 5 a). Mtoto ameshiba mno*
*b). Sherehe za mahafali zimerudi tena.*
**Chanzo:** Data ya Uwandani (2023)

Katika data hizo, tunaona kuwa sentensi ya Mt. 5(a) imetumia “mno” kama kisisitizi cha sentensi. katika sentensi ya Mt. 5(b) imetumia “tena” kama kisisitizi cha sentensi. Kutumika kwa vielezi hivyo katika sentensi kumeonesha nia ya taarifa fulani. Katika sentensi ya Mt. 5(a) kusudio la msemaji ni kuonesha kuwa mtoto huyo anayezungumziwa amekula chakula kingi kiasi cha kumfanya ashibe kupitiliza. Kielezi asilia “mno” ndiyo msingi wa kusudio la msemaji wa usemi huo. Si hivyo tu katika sentensi ya Mt. 5(b) msemaji ametumia kielezi asili “tena” kuonesha dhamiraya usemi wake. Kusudio la msemaji katika sentensi hiyo ni kuonesha kuwa, sherehe hizo zilikuwapokabla lakini zilisimama kwa muda na sasa zimeanza kufanyika. Kwa hiyo, kuwepo kwa kielezi hicho kinaonesha kusisitiza kuhusu kuanzishwa kwa mara nyingine sherehe hizo. Katika kusisitizaufafanuzi wa data hapo juu Nadharia ya Uchunguzi wa Kimaeneo inaeleza kuwa mzungumzaji anapaswa kutumia lugha kulingana na lengo ili kuendana na muktadha wa usemi au mazungumzo husika. Hivyo, lugha isipotumika sahihi husababisha kupotoka kwa kusudio la msemaji wa usemi kwa wasemaji kupata maana isiyokusudiwa na mzungumzaji. Kwa hiyo, data hizo zinaonesha waziusisitizi kwa kutumia vielezi asilia vilivyotumika katika tungo hizo. Hivyo, vielezi asilia hutumika katika muktadha wa usisitizi kutokana na makusudio ya mawasiliano. Miundo ya vielezi asilia katika sentensi hizo imejitokeza wazi baada ya vitenzi si elekezi kuonesha hiyo ni taarifa ya ziada.

### 4.1.3 Muktadha wa Uulizi/ swali

Kwa mujibu wa Kamusi Kuu ya Kiswahili (2022) ulizo ni kauli inayohitaji jibu. Kuuliza ni hali ya kutaka kupata taarifa au kufahamu jambo kutoka kwa mtu. Katika kusudio hili, viulizi hutumika katika sentensi andishi. Katika mazungumzo, viimbo hutumika kuonesha uulizaji au swali. Utafiti huu ulishughulika na uulizi unaotokana na viulizi katika maandishi. Katika lugha ya Kiswahili kuna viulizi tofauti kulingana na dhamira ya usemi husika. Kuna viulizi vya muda, sababu na mahali. Baadhi ya viulizi vinavyotumika ni je, kwa nini, nini, nani, wapi, lini, gani, ngapi, n.k. Uulizaji ni miongoni mwa miktadha ya kisintaksia kwa sababu husababisha mabadiliko ya kimuundo katika sentensi. Katika utafiti huu imebainika kuwa, viambajengo vinavyotumika katika uulizi huibua miundo tofauti ya sentensi za Kiswahili. Tazama data ifuatayo kutoka kwa Mt. 6 na Mt. 7:

*Mt.6 na 7 a). Je, mvua za Elinino zimeshaanza?*
*b). Kwa nini wanafunzi wamechelewa kuripoti chuoni?*
*c). Ni lini, mbunge wetu wa Mororgoro Mjini atateuliwa kuwa waziri kama wabunge wengine?*
*d). Hivi ni wajumbe wangapi walioteuliwa kuwa wazee wa baraza la mahakama kuu?*
**Chanzo:** Uwandani (2023)

Katika data hapo juu tunaona sentensi zimeanza na viambajengo vya kuulizia ambavyo ni "je", "kwa nini", "lini" na "ngapi". Viambajengo hivyo vimetumika katika sentensi hizo kwa lengo la kuonesha kusudio la kuuliza. Katika sentensi ya kwanza kiuliizi "je" kimetokea mwanzoni mwa sentensi. Kuwapo kwa kiulizi hicho kunaashiria moja kwa moja kuwa kusudio la usemi huo ni kuuliza. Lakini si lazima katika kila kusudio hili kiulizi hicho hutokea mwanzoni kuna wakati huweza kutokea mwisho mwa sentensi mfano; shule ya sekondari Kayenzi inafanya vizuri sana katika michezo, Lupanga je? Katika sentensi ya pili kiulizi "kwa nini" kimetumika kuwakilisha kusudio la kuuliza ili kupata taarifa ambayo msemaji anaikusudia. Pia, katika sentensi ya tatu kiulizi"lini" kimetokea katikati ya sentensi na sentensi ya mwisho kiulizi "ngapi" kimetokea katikati ya sentensi. Katika kusudio hili viulizi huweza kutokea mwanzoni mwa sentensi, kati au mwishoni hutegemeana na mpangilio wa usemi wa msemaji. Katika Nadharia ya Uchunguzi wa Kimaene oinasisitizwa kuwa, ni muhimu kuzingatia dhamira ya msemaji katika mazungumzo kwa kuwa na mpangilio sahihi wa maneno ili kudhihirisha kusudio la msemaji. Hivyo, makusudio ya mawasiliano ndiyo yanayoweza kusababisha mpangilio wa sentensi yaani, miundo ya sentensi. Ikiwa kusudio ni kuuliza, mwandishi hana budi katika mpangilio wa sentensi hiyo ni lazima uteue kiulizi chochote miongoni mwa viulizi husika ili kukamilisha kusudio hilo. Lakini si hivyo tu uteuzi wa kiulizi ni lazima uendane na usemi husika kwa sababu si kila kiulizi kuweza kukaa katika sentensi yoyote. Nadharia hii inakubaliana kuwa msemaji anapaswa kuzingatia lengo la usemi anapokuwa katika muktadha wa mazungumzo kwa kuwa na uteuzi sahihi wa maneno ili aweze kufikia dhamira ya mazungumzo yake. Katika data hizo, tumeona kuna miundo tofauti ya sentensi hizo kwa sababu ya ujitokezaji tofauti wa viulizi hivyo.

## 4.1.4 Muktadha wa Ombi

Kwa mujibu wa Kamusi Kuu ya Kiswahili (2022) kuomba/ombi ni matakwa anayoyatoa mtu kwa maneno au ishara kwa mwenye uwezo wa kumsaidia. Lakini kuomba inaweza kuwa ni kitendo cha kutaka ridhaa ya mtu katika kufanya jambo au kuchukua kitu kutoka kwake. Imebainika katika sentensi za lugha ya Kiswahili, maombi hutawaliwa na maneno maalumu ambayo hutumikamwanzo kati au mwisho wa sentensi. Maneno hayo ni kama vile: tafadhali, nisaidie, naomba n.k. Utumizi wa maneno ya kuomba yana mchango mkubwa katika kuibua miundo ya sentensi za Kiswahili. Hivyo, huu ni miongoni mwa miktadha ya kisintaksia inayotokana na dhamira hiyo kwasababu una athari moja kwa moja na miundo ya sentensi za Kiswahili. Tuchunguze data zifuatazo kutoka kwa Mt. 8 na Mt. 9:

Mt.8 na 9 *a). Tafadhali tunaweza kuonana leo*
*b). Naomba ukipata nafasi tuonane chuoni*
*c). Mwamvua unaweza kunisaidia kazi yangu.*
**Chanzo:** Uwandani (2023)

Katika data hizo hapo juu sentensi ya Mt. 8 na Mt. 9 (a), (b) na (c) zinaonesha maneno ambayo hutumika katika kusudio la kuomba. Sentensi ya kwanza imetumia neno "tafadhali" kuonesha dhamira ya msemaji kuwa ni kuomba ridhaa ya mtu.

Pia, sentensi ya pili imetumia neno "naomba" kuonesha dhamira ya msemaji kuwa ni kutaka kitu kutoka kwa mtu, pia, sentensi ya mwisho imetumia "unaweza kunisaidia" kuonesha kuwa msemaji ana dhamira ya kuhitaji msaada. Kusudio hili hudhihirika wazi kutokana na maneno yanayotumika katika usemi husika. Msikilizaji hubaini waziwazi dhamira ya msemaji kuwa ni kuomba kutokana na namna maneno yalivyoteuliwa na kupangwa. Kama inavyoelezwa na Nadharia ya Uchunguzi wa Kimaeneo kuwa, uzingativu wa lengo la msemaji ni muhimu kwani ndiyo linalochochea kusudio la msemaji kwa kuweka mtiririko mzuri wa maneno. Msemaji anapaswa kuonesha dhamira yake kwa kuweka mpangilio mzuri wa usemi wake. Ukichunguza data hapo juu utagundua kuwa, baada ya kutumia maneno ya kuomba katika muktadha wa ombi, muundo wa sentensi umekuwa wa aina yake. Kwani ukichunguza sentensi hizo utagundua kuwa vitenzi viwili na zaidi vimefuatana kuunda sentensi hizo. Mfuatano huu wa vitenzi sio wa bahati mbaya bali umeibuka kwa sababu ya muktadha wa kisintasia wa ombi. Ufafanuzi wa muundo huo utaelezwa katika uchambuzi wa lengo la pili la utafiti huu.

### 4.1.5 Muktadha wa Kuagiza

Huu nao ni sehemu ya muktadha wa kisintaksia unaoibua miundo katika sentensi za Kiswahili. Kwa mujibu wa Kamusi Kuu ya Kiswahili (2022) kuagiza/agiza ni kitendo cha kutoa amri ya kutendeka kwa jambo. Pia, kuagiza inaweza kuwa ni kuamuru mtu au watu kufanya jambo ambalo unahitaji. Imebainika katika sentensi za lugha ya Kiswahili, uagizaji hutawaliwa na muundo maalumu wa vitenzi. Vitenzi vinavyotumika kwenye kuagiza huwa vina sifa ya kuondoa mofu tangulizi au kutumia tu mofu ya nafsi kama kitenzi hicho kitakuwa ni bebwa. Tuchunguze data zifuatazo kutoka kwa Mt. 10:

*Mt. 10* *a). Nenda shambani haraka*
*b). Mwambie aende leo na sio kesho*
*c). Peleka madaftari ofisini sasa hivi*
**Chanzo**: Uwandani (2023)

Katika data hapo juu tunaona kuwa sentensi ya Mt. 10 (a) imetumia kitenzi cha kuagiza kisichokuwa na mofu tangulizi "nenda" kitenzi hicho kinafanya kazi ya kuamuru mtu kufanya jambo linalomaliziwa na sentensi hiyo shambani haraka. Katika sentensi ya Mt. 10 (b) imetumia kitenzi "aende" ambacho kimeundwa na mofu ya nafsi lakini ukichunguza kitenzi hicho kinafanya kazi sawa na kitenzi kilichotumika katika sentensi ya Mt. 10 (a). Katika sentensi ya mwisho imetumia ambayo ni sentensi ya Mt. 10 (c) kitenzi "peleka" kuonesha dhamira ileile ya kuamuru kama ilivyokuwa katika mifano ya awali. Data hii inatusaidia kufahamu kuwa katika lugha ya Kiswahili vipo vitenzi kadhaa vinavyofanya kazi ya kubeba dhamira ya kuagiza. Utumizi wa vitenzi hivyo hutegemea makusudio ya mawasiliano kama inavyofafanuliwa na Nadharia ya Uchunguzi wa Kimaeneo kuwa, ili kubaini kusudio la usemi wowote katika sentensi ni muhimu kuwe na uzingativu wa uteuzi wa maneno kwa makusudio maalumu. Kinachosisitizwa hapa ni kuwa dhamira ya mawasiliano ndio inayosukuma uteuzi wa vitenzi maalumu ambavyo vinaendana na kusudio la usemi huo. Si kila kitenzi kinaweza kukukusudia kuonesha agizo. Hivyo, msemaji anapaswa kuwa mbunifu kuweza kutambua vitenzi sahihi kulingana na kusudio lake kama ilivyodhihirishwa katika data hizo. Ukifuatilia miktadha ya kisintaksia iliyoainishwa hapo juu ni miktadha ambayo ina mchango mkubwa wa kuibuka miundo tofauti ya sentensi za Kiswahili. Miundo hiyo ndio inayokusudiwa kufafanuliwa katika lengo la pili linalofuata katika utafiti huu.

## 5.0 **Hitimisho**

Makala haya yaliangazia kuhusu miktadha ya kisintaksia inayotokana na makusudio ya mawasiliano katika lugha ya Kiswahili. Matokeo ya makala haya yamebainisha kuna aina sita za miktadha ya kisintaksia inayotokana na makusudio ya mawasiliano katika lugha ya Kiswahili ambayo huwa na sentensi zenye miundo tofauti kulingana na kusudio la msemaji. Miktadha hiyo ni umadaishaji, ufokasilishaji, usititizi, uulizi, maombi na kuagiza. Imegundulika kuwa, muktadha wa umadaishaji ni muktadha wa kisintaksia ambao hutokana na utumizi wa viambajengo kwenye nafasi ya mwanzo katika sentensi. Kisintaksia, kiambajengo kwenye nafasi ya mwanzo ndicho kinachopewa hadhi kubwa, ndicho kinachorejelewa na sentensi hiyo. Muktadha wa usisitizi ni ule muktadha unaotokana na msemaji kutumia maneno au sentensi ambayo inamfanya msikilizaji aone kuwa kuna jambo lililoshadadiwa zaidi katika hayo mazungumzo. Kutokana na datazilizokusanywa na utafiti huu, imegundulika kuwa, muktadha wa kisintaksia wa usisitizi unaweza kujitokeza katika mpangilio wa sentensi kwa njia ya uradidi, njia ya upangaji maalumu waviambajengo katika sentensi na njia ya utumizi wa maneno maalumu katika sentensi. Muktadha mwengine uliobainika ni muktadha wa ufokasilishaji ambao ni muktadha wa kisintaksia unaouhusuukamilishaji wa taarifa katika sentensi. Imegundulika kuwa ufokasilishaji hujitokeza baada ya kitenzi. Vipashio vinavyotumika kukamilisha taarifa baada ya kitenzi huweza kuwa kirai nomino, viwakilishi vya kirai nomino na hata sentensi bebwa. Iligundulika pia, kuna muktadha wa uulizi ambao ni muktadha wa kisitanksia unaotokana na utumizi wa viulizi tofauti katika sentensi. Imegundulika kuna viulizi vya muda, namna, sababu na mahali. Baadhi ya viulizi vinavyotumika nije, kwa nini, nini, nani, wapi, lini, gani, ngapi, n.k. Pia, uligundulika muktadha wa ombi ambao ni muktadha wa kisintaksia unaotumia maneno maalumu ya kuomba katika sentensi. Maneno hayo huweza kutumika mwanzo kati au mwisho wa sentensi. Maneno hayo ni kama vile: tafadhali, nisaidie, naomba n.k. Muktadha wa mwisho uliogundulika na utafiti huu ni muktadha wa kuagiza. Huu ni muktadha wa kisintaksia unaotumia maneno ya kuamuru (hasa vitenzi) kwenye mpangilio wa sentensi. Imebainika kuwa vitenzi vinavyotumika kwenye kuagiza huwa vina sifa ya kuondoa mofu tangulizi au kutumia tu mofu ya nafsi kama kitenzi hicho kitakuwa ni bebwa.

## Marejeleo

BAKITA, (2022). Kamusi Kuu ya Kiswahili. Nairobi: Longhorn Publisher. Denscombe, M. (2002). Ground Rules Good Research: A 10 Point Guide for Social Research. United Kingdom: Open University Press.

Fishman, J.A. (1972). Language in Sociocultural change. (Dil, Anwar S. Ed). California: Stanford University Press.

Fishman, J.A. (1972). The Sociology of Language: An Interdisciplinary Social Science Approach to Language in Society. California: Newbury Rowley.

Halliday, M.A.K. (1967). Notes on Transitivity and Theme in English. Journal of Linguistics. Juz. 3:37-245.

King'ei, K. (2010). Misingi ya Isimujamii. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam.

Kingei, K. (2014). Taaluma ya Uandishi. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation. Kombe, L. (2019). Uchambuzi wa Sintaksia ya Uambatanishaji katika Lugha ya Kiswahili. Tasnifu ya Uzamivu. Chuo kikuu cha Dar-es-salaam.

Kombo, D.K. (2006). Proposal and Thesis Writing. An Introduction. Nairobi: Pauline Publication African.

Kothari, C.R. (2009). Research Methodology: Methods and Techniques. New Delhi: New Age International Publishers Limited.

Lambrecht, K. (1994). Information Structure and Sentence Form: Topic, Focus, and Mental Representation of Discourse Referents. Cambridge: Cambridge University Press.

Massamba, D. (2009). Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha. Dar-es-salaam: TUKI. Ndung'u, N.M. (2015) "Information Structure in Kiswahili". International Journal of Education and Research. Juz. 3(3): 309-320.

Ponera, A.S. (2019). Misingi ya utafiti wa Kitaamuli na Uandishi Tasnifu. Dodoma: Central Tanganyika Press. Stanford University Press. Tavakoli, Hossein. (2012). A Dictionary of Research Methodology and Statistics in Applied Linguistics. Rahnama Press

Tuki (2013). Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha. Dar-es-salaam: Tuki.

Tuki (2014). Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Dar-es-salaam: Tuki. Wanjala, F.S na Kavoi, J.M. (2013). Stadi za Mawasiliano na Mbinu za Kufundisha Kiswahili. Mwanza: Serengeti Educational Publishers Ltd.

Wesana-Chomi, E. (2017). Muundo wa Viambajengo wa Sentensi za Kiswahili.